Pasteur Kitoka Moke Mutondo

# MBINU ZA KULETA WATU KWA YESU

Kitabu cha Mwinjilisti

## Sommaire

KIINGILIO.....3

UTANGULIZI..... 5

1. WATU WASIOJALI WOKOVU..... 7
2. WATU WANAO TAFUTA WOKOVU AO MSAADA..... 8
3. WATU WANAO TAFAKARI.....8
4. WANAO JIZANIA KUWA WATAKATIFU, WASIO NA DHAMBI.....10
5. WAKRISTO WA JINA, WALIO ANGUKA.....11
6. WAPAGANI WANAO MKANA MUNGU.....12
7. WATU WANAO PENDA UBISHI.....12
8. WATU WANAO PIGA HESABU.....13

KWA MWISHO.....14

## KIINGILIO

Mbele ya kupaa mbinguni, Yesu aliwaagiza wanafunzi wake wasitoke Yerusalemu, bali wangoje Roho Mtakatifu (Matendo 1 : 4-5). Kusudi lake ilikuwa kuwatayarisha kwa kazi aliyo wapatia : Kwenda ulimwenguni pote na kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi wake (Matayo 28 : 19- 20).
Katika agizo hili, Yesu alipenda kukumbusha mitume kwamba mpango wa Mungu ni kwamba kila mwanadamu aokoke na kuwa kiumbe kipya.

Baada ya kupokea Roho siku ya Pentekoste, mitume walianza kupasha habari njema na Kanisa lilianza. Umbalimbali na mafikiri ya wengi, kuleta watu kwa Yesu sio kazi ya wainjilisti peke yao ; ila ni kazi ya kila mkristo.

Katika mpango wakusaidia kila kikundi kufanya huduma yake katika kumpendeza Mungu, Mchungaji wa kanisa la 8ème CEPAC CHAHI, Révérend SHINDANO MASILYA aliomba kila kikundi ya huduma lipate mafundisho itakayo wasaidia kuleta mchango wao kwa maendeleo ya kanisa letu. Katika somo hili, kusudi letu ni kuonyesha wakristo wa kanisa la Chahi kwa jumla na wainjilisti kwa upekee namna ya kuleta watu kwa Yesu. Somo hili ni mojawapo wa mbinu za kusaidia kila kikundi cha huduma kanisani kuelewa jukumu lake, namna ya kuifanya na nini itamusaidia kuifanya (programme élargi de renforcement des capacités des différents groupes ministériels).
Ni lazima tuonyeshe kwamba, katika kutangaza habari njema, mara nyingi maneno yetu hayaguse watu sababu tunatumia maandiko matakatifu (versets bibliques) ki holela, bila kujua nani tunaweza kutumia shairi gani la Biblia. Kila mwanadamu anakuwa tofauti na mwengine na nilazima mupashaji habari njema afahamu namna gani kuvuta kila mumoja kufuatana na hali.

Kunakua mbinu nyingi za upashaji wa habari njema (hazarani, kwa miradi ya maendeleo, kupitia redio na télévision, …). Katika somo hili tunaonyesha mbinu ya nyumba kwa nyumba ao mtu kwa mwengine. Mbinu hii inaonekana ya muhimu katika miji mikuu kama huu wa Bukavu sababu watu wengi hawana muda kwenda kufuata mahubiri hazarani na wengi wanaitaji neno linalo gusia hali yao binafsi. Ndio sababu tunaonyesha hali mbalimbali za watu ambao tunaweza kukutana nao katika huduma yetu ya kuleta watu kwa Yesu.

Ni lazima tuonyeshe kwamba haiwezekane kuonyesha hali zote za watu katika somo, ila tumetiwa moyo tukumbukapo kwamba Mungu anayetutuma kupasha habari njema, anajua hali ya kila mwanadamu na maitaji yake.

Tunaleta shukrani zetu kwa Mzee Alexis WAKULABWAMI aliye soma na kuleta maonyi yake kusudi kitabu hiki kiwe na swahili nzuri. Asante pia kwa muke wangu Alphonsine aliye andika na kusaihisha somo hili kwa ordinateur.

**UTANGULIZI**

Kuleta watu kwa Yesu sio jambo raisi, na halipashwe kufanyika kwa mapenzi na nia ya mtu binafsi. Ni lazima yule anaye fanya huduma hii awe mtu mwenye kuzaliwa mara ya pili na kuitwa na Mungu kufanya kazi hii. Yesu alipowaita Petro na Andrea, aliwaambia waziwazi ya kwamba anawaita ili wawe wavuvi wa watu (Matayo 4 : 18-19). Bila mwito toka Mungu haiwezekane kufaulu katika huduma ya kuleta watu kwa Yesu, sababu inahitaji juudi, uwezo, uvumilivu na upendo wa mioyo iliyo potea katika dhambi. Katika maisha yake, ni lazima kila mkristo afahamu ni nani aliye muita, namna gani aliitwa, aliitwa kufanya nini na kuchunguza ikiwa anatumikia Mungu namna inavyo mupasa.

Katika semina ya mashemasi, tulionyesha mambo mengi kuhusu mwito na kutia mkazo kuhusu ujazo wa Roho Mtakatifu na maisha ya utakaso kama nguzo ya kufaulu katika huduma yeyote kanisani. Kama huduma zingine, upashaji wa habari njema ina shurti na kanuni zake. Tukiwa wenye kuongozwa na Roho Mtakatifu, mambo yatakuwa raisi kwetu. Japokua kuleta watu kwa Yesu ni kazi na mapashwa ya kila mukristo, ni lazima, mbele ya kuanza kazi ya évangélisation, atimize shurti zi fuatazo :

- ❖ Kwa kufaulu katika huduma ya kuleta watu kwa Yesu, inabidi évangéliste awe amekwisha zaliwa mara ya pili bi nafsi. Yesu alimuambia Petro ya kwamba, ukisha geuka, utahimiza ndugu zako. Nivigumu kwa mtu kuleta wengine kwa Yesu ikiwa yeye peke bado kuacha dhambi na kuachana na mambo ya dunia.
- ❖ Kwa kuleta watu kwa Yesu, ni lazima kuwa na upendo kwa mioyo iliyopotea ; yaani ni lazima kuwa na huruma kwa watu wasio mjua Kristo na wanao ishi katika dhambi. Hata kama tunajikaza, tusipokuwa na upendo kwa watu wanao ishi katika dhambi, hatuweze kuwaleta kwa Yesu. Sababu upendo ni tunda la Roho, ni lazima kwetu kuomba roho ya upendo, ni lazima tumuombe Mungu atupatie roho ya upendo (1Yohana 5 : 14-15 ; Wafilipi 4 : 19), sababu Yesu mwenyewe alikuwa na roho ya upendo kwa mioyo iliyo potea (Matayo 23 : 37 ; Luka 19 : 10)
- ❖ Kwa kuleta watu kwa Yesu, nilazima mwinjilisti afahamu vema neno la Mungu na kujua kulifundisha namna ipasavyo ( 2 Timoteo 2 : 15). Neno la Mungu ni upanga wa Roho Mtakatifu (Waefeso 6 : 17), ndio chombo Mungu analotumia kwa kupasua mioyo migumu na kuhakikishia wapagani kwamba wanahitaji wokovu. Ni lazima kwa mwinjilisti ajue kulitumia kwa :

- Kuwahakikishia wanadamu kama wanahaja ya mwokozi,
- Kuwaonyesha kwamba Yesu ndiye mwokozi anaye wafaa,

- Kuwafunza wamufuate Yesu kuwa bwana na mwokozi wa maisha yao binafsi,
- Kuwasaidia kuachana na ile inayowazuia kumukubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao.

❖ Kwa kuleta watu kwa Yesu inaomba kuwa na muda mwingi wa maombi. Kwa kutayarisha mioyo itakayo hubiriwa kupokea Yesu, inaomba saa nyingi za maombi na kuomba Mungu:

- Akuongoze kwenye mioyo unayopashwa leta kwa Yesu. Hatupashwe ku hubiri kila mtu tunaye kuta njiani; ni Mungu ndie anajua wale wanao pashwa kuelezwa habari njema na nilazima tuombe uongozi wake (Matenda 8: 29)
- Atuonyeshe nini tunapashwa ambia wale ambao anatutuma kwao. Hata kama tunajua mashairi ya biblia (versets bibliques), hatupashwe kuzitumia hovyo hovyo sababu kila mtu anahitaji maandiko yake.
- Abariki ujumbe alitupatia kwa watu tunaozungumza ili apake neno lake mafuta na uwezo ili lipate kuwagusa.
- Baada ya kuzungumza na mtu ni lazima tuendelee kumuombea ili Roho Mtakatifu aendelee kumuangazia.

❖ Kwa kuleta watu kwa Yesu, ni lazima mwinjiliste awe mwenye kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba nilazima wangoje Yerusalemu mbele ya kuanza huduma yeyote. Na ni baada ya Pentekoste ndio walianza huduma yao.

Baada ya kutimiza shurti hizi, ni lazima kujifunza namna ya kuwaendea watu na kuwapasha habari njema. Ni raisi kuzungumzia mtu aliye ingia kanisani, kunako mkutano wa kikristo ao katika jamaa la kikristo. Sio raisi kuanza kupasha habari njema kwa mtu usiye mjua wala usiye zoea. Ndio sababu ni lazima kujifunza namna gani kuanza mazungumuzo naye. Mara nyingi tunaweza kuanza na:

- Kuzungumuzia mada (mambo) inayosemeka na watu wote katika mjini (Habari za masomo kutofunguliwa, habari ya prime kwa masomo, kupanda kwa vitu sokoni, wizi na mauwaji iliyo pitika fasi furani, habari za radio,…) na baadaye ndio tunaingiza mazungumuzo kuhusu habari njema sawa vile Yesu alifanya na Muke mu Samaria (Yohana 4: 1- 42). Alianza na kuomba maji ya kunywa na akamalizia na habari njema.
- Baada ya mazungumuzo kuhusu mada Fulani, nilazima sasa kuuliza kama yeye ni Mkristo ao hapana. Inatubidi kuuliza ulizo hili na adabu na bila mizaa.
- Mara zingine inabidi kuanza na kutafuta yule tunayependa leta kwa Yesu atuaminie (awe na confiance na sisi) ao atufurahiye kwanza mbele ya kumupasha habari njema. Kupitia mwenendo wetu, ushuhuda wetu, namna tunavyo ishi nao, tabia zetu, usemi wetu, kazi

yetu, wapagani wanaweza kutuaminia. Baada ya kutuamini, tunaweza sasa kuwazungumzia kuhusu Kristo.

- Traité ao kitabu inaweza pia kutumiwa kwa kuleta watu kwa Yesu. Tunapo patia mtu traité, ao kitabu kuhusu maisha ya kikristo na ya ulimwengu, tunaweza kuzoeana naye na kumuleta kwa Kristo. Mara nyingi wa Témoins de Jehova wanagawanya vitabu kwa bure ili wazoeane na watu na siku moja watawazungumzia Jehova.

Baada ya hatua hizi, nilazima kujihazari na kutumia mashairi ya Biblia hovyo hovyo. Inamupasa évangéliste afahamu nani anaye zungumuza naye, ni wa hali gani kusudi ajue pia Verset ao shairi gani mtu yule anastahili kupewa kusudi avutwe kwa Yesu.

Mara nyi ngi, kuna aina kenda (9) ya watu ambao mara kwa mara mwinjilisti anakutana nao katika huduma yake na nilazima ajue kila aina na neno linalo wapasa.

## 1. WATU WASIOJALI WOKOVU

Kundi hili ni lenye kuwa na watu wengi. Mara nyingi watu wengi hawajali maana ya kuwa na mwokozi katika maisha yao wakifikiri kwamba hawahitaji kuokolewa. Kwa kuwavuta kwa Yesu, nilazima kuwasaidia kuelewa kwamba wao ni wenye dhambi na wanahitaji kuokolewa. Kwa hivi unaitaji kuwasomea **Waroma 3: 23**: *Kwa sababu **wote** wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*. Ni vizuri kumpa yeye peke Biblia ili asome mwenyewe maneno haya. Na baadaye umuulize: **Nani** amefanya dhambi? Na umusaidie kujibu **WOTE** ili ajikute kwamba hata yeye pia ni mwenye dhambi. Umusaidie sasa kusoma: *kwa sababu **nimefanya** dhambi na nimepungukiwa na utukufu wa Mungu.* Unaweza pia kutumia Isaya **53: 6**: *Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mumoja kwa njia yake mwenyewe*. *Na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.* Umpe maulizo mpaka ajitambue na kuelewa kama *yeye* ni mmoja wa zile kondoo zilizo potea. Baadaye umuulize nini ndio Yesu alimufanyia kusudi akiri kwamba ni Yesu ndiye alichukuwa dhambi zake. Unaweza baadaye kumuuliza: Je unakubali kumpokea kama mwokozi yule aliye chukua dhambi zako?

Unaweza pia kumusomea **Zaburi 130: 3** inayosema: *Kama wewe Bwana ukihesabu maovu, Ee Bwana, nani ataishi?* Unaweza pia tumia **Matayo 22: 37-38** na kumuonyesha kwamba kabla haja mpokea Yesu kama Bwana na mwokozi wa maisha yake, amevunja amri kubwa ya Mungu, na amefanya dhambi iliyo kubwa kuliko zingine zote.

Mbele ya watu wasio jali, unaweza pia tumia **Waroma 6: 23** na kuonyesha kwamba Mshahara wa dhambi ni mauti na kumuuliza *mshahara wa dhambi ni nini?, wewe ni mfanya dhambi ? Mshahara wako nini?* Kiisha umpe asome Yohana 3: 36 ili avumbue kwamba *anaye amini mwana ana uzima wa milele; na asiyetii Mwana hataona uzima, lakini gadhabu ya Mungu*

*inakaa juu yake.* Unaweza pia tumia 2 Watesalonika 1: 7-9; Yohana 8: 24; Ufunuo 20: 15; 21: 8; 14: 10- 11; Isaya 53: 5-6 na Yohana 3: 16; 1 Petro 2: 24; Waebrania 10: 28-29; Isaya 57: 21.

**2. WATU WANAO TAFUTA WOKOVU AO MSAADA**

Kundi hili ni la watu wenye shida na matatizo na ambao wanatafuta nani atakaye wasaidia katika shida zao. Watu kama hawa si vigumu kuwaleta kwa Yesu. Andiko linalo faa kwao zaidi ni lile la Isaya 53 : 6 inayo onyesha wazi njia ya wokovu. Unaweza pia tumia Isaya 55: 7; Matendo 16: 31; Yohana 3 : 16; 3 : 36; Yahana 3: 14 ukimuuliza ikiwa anakubali kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake binafsi ? Maandiko mengine ni yale ya Waroma 1: 16 itakusaidia kuonyesha mtu mwenye kutafuta msaada kama ana jambo moja tu la kufanya: kuamini habari njema. Kwa kumsaidia kuelewa habari njema ni nini, tumia 1 Wakorinto 15: 1- 4. Baadaye umuulize ikiwa anaamini kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zake? Akihakikisha, umuulize je, anamukubali kama Bwana na Mwokozi wake? Kwa kumueleweshe maana ya wokovu, unaweza tumia Warumi 10: 9-10; 10: 13. Luka 18: 10- 14 inaonyesha nini mwanadamu (mfarisayo) anaye potea na nini kile mtu anaye kosea wanaweza kufanya kwa kuokolewa. Luka 7: 48- 50 inaonyesha vizuri mfano wa imani.

**3. WATU WANAO TAFAKARI**

Kundi ni la watu ambao, pamoja na kuwa na hamu ya wokovu wanakuwa na vizuizo vingi ambavyo wanashindwa kuviacha. Mara kwa mara wanatoa sababu zifuatazo:

- Mimi ni mwenye dhambi nyingi sana, mimi ni mtu mbaya, nimekwisha tenda mabaya mengi hata Mungu haweze kunisamehe. Wanao jibu hivi, uwape wasome 1 Timoteo 1: 15 *Neno hili ni la kuaminiwa, tena lastahili kukubaliwa na watu wote, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuokowa wenye dhambi, na mimi, wa kwanza wao.* Kiisha umuonyeshe kwamba ni kwa ajili yake ndio Kristo alikuja ulimwenguni ili amuokoe yeye binafsi. Akiendelea na mashaka, umpe asome pia Waroma 5: 8 *Lakini Mungu anaonyesha upendo wake kwetu, wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.* Baadaye umuambie, ndio, unasema wewe ni mwenye dhambi nyingi na andiko hili linazungumzia upendo wa Mungu kwa wenye zambi. Unaweza tena kutumia Warumi 10: 13 ukitia mkazo kwenye neno *kila*. Tumia pia Matayo 9: 12-13; Isaya 1: 18; 1 Yohana 4 : 14; 1 Yohana 2 : 1-2; Isaya 44 : 22; 43: 25. Ikiwa mtu unayezungumza naye ni muuwaji changa Matayo 9: 12 – 13 na Zaburi 51 : 1- 14;
- Sitashinda kudumu katika maisha ya kikristo bila kuanguka katika dhambi. Kwa jibu hili tumia 1 Petro 1: 5 inayo onyesha kwamba hatujichunge wenyewe ila ni Mungu anayetuchunga na kutuwezesha kwa uwezo wake. Yohana 10: 28-29 inatuonyesha kwamba usalama wa yule aliye mkubali Yesu unalindwa na Mungu baba na Mwana. 2 Timoteo 1: 12 inaonyesha kwamba ni Yesu peke yake ndiye ujihusisha na kulinda lile

tulilo mpatia. Unaweza pia tumia Isaya 41: 10, 13 ; 2 Mambo ya nyakati 32 : 7-8; Warumi 14 : 4; 2 Watesalonika 3 : 3; 1 Wakorinto 10: 13; 2 Wakorinto 12 : 9- 10.

- Mimi ni mdhaifu kiroho na si raisi kwangu kuamua leo, nitafikiri kwanza na nitakujibu siku ingine sababu inaomba kuchukua uamzi ngumu. Kwa watu kama na hawa tumia 2 Wakorinto 12: 9 – 10 na umuulize: Nguvu za Kristo zinaonekana wapi? Atakapo kujibu *katika udhaifu*, umueleze kwamba *kila mara anapojitambua kuwa mdhaifu kwa macho yake binafsi, nguvu za Kristo zinaongezeka na kujizihirisha.* Wafilipi 4 : 13 inaonyesha pia kwamba hata kama tu wazaifu wa aina gani, tunaweza yote kwa Kristo atutiaye nguvu. 1 Wakorinto 10 : 13 inatuhakikishia kwamba *Mungu anajua udhaifu wetu na hataruhusu tujaribiwe kuliko nguvu zetu.*
- Mimi siweze tena kuacha tabia zangu mbaya na dhambi zangu. Watu wanaokujibu hivi uwape wasome Wagalatia 6 : 7 – 8 inayosema kwamba *Mungu hadhihakiwi na lolote alipandalo mtu ndilo atakalo livuna.* Wafilipi 4 : 13 inaonyesha kwamba watawezeshwa kwa nguvu za Kristo. Nilazima pia kuwaonyesha Kristo aliye fufuka (1 Wakorinto 15: 3-4.
- Nikiamini Kristo nitateswa na kuchukiwa na watu. Usiwaambie kwamba hawata teswa, ila uwaonyeshe kwamba mateso ndio njia ya utukufu ukitumia 2 Timoteo 2: 12; 3: 12; Matayo 5: 10-12; Marko 8 : 35; Matendo 14 : 22; uwaonyeshe pia **Waroma 8 : 18** uwaeleweshe andiko hili ukitumia Matendo 5 **:** 41 na 1 Petro 2: 20 – 21 ukiwaonyesha kwamba ni faida kuteswa kwa ajili ya Kristo. Waebrania 12: 2-3 inatuonyesha ni nani tunayeweza kutegemea kwa kushinda wakati wa mateso.
- Nikiamini kazi yangu itaharibika ao kazi yangu hainiruhusu kuwa mukristo. Watu wanao kujibia hivi uwape wasome Marko 8 : 36 ina onyesha kwamba *ni heri kupoteza feza kuliko kupoteza nafsi yako.* Baada ya kutia mkazo kuusu neno hili, umupe asome pia Matayo 6: 32 – 33 inayo muomba kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake na mengine yote atatuongezea mengine tunayo hitaji. Unaweza pia kutumia Matayo 16 : 24 -27; Luka 12 : 16 – 21; 16 : 24-26.
- Ukristo unaomba mtu aache vitu vingi sana, ukristo unamashurti mingi sana. Mtu anapokujibu hivi, umpe asome Marko 8: 36 inayo onyesha kwamba ni heri kuacha yote kuliko kupoteza nafsi yako. Wafilipi 3: 7-8; Zaburi 16: 11 itawaonyesha kwamba yale watakayo acha si ya muhimu kuliko ile watakayo pata baadaye. Zaburi 84 : 11; Waroma 8: 32 inawaonyesha kwamba Mungu hatawaomba kamwe waache ile iliyo nzuri kwao ila ile inayoweza kuzuru maisha yao.
- Ninaogopa kuzarauliwa na kulaumiwa na rafiki zangu. Watu wanaojibu hivi wanaogopa kupoteza ao kukataliwa na marafiki zao. Mezali 29 : 25 itawasaidia kufaamu matokeo mabaya ya woga wao na salama wanayo wale wanao mcha Mungu. Mezali 22: 24 – 25

itawajulisha wapi marafiki wabaya wanawapeleka. Unaweza pia kuwapa wasome Zaburi 1 itakayo waonyesha faida ya kuachana na marafiki wabaya. 1 Yohana 1: 4 itamuonyesha kwamba watakuwa na faida kubwa zaidi katika kuachana nao.

- Moyo wangu ni mgumu sana. Mtu unaye penda kuleta kwa Yesu akikupatia jibu ili, umpatie asome Ezekieli 36 : 26 – 27, ina onyesha kama Mungu anaweza kuwapa moyo mpya utakao komboa ule mgumu.
- Nimekwisha choka na kumtafuta Yesu wala simpate. Mtu anapo kujibu hivi, umpe asome Yeremia 29 : 13 na Mezali 8 : 17 inayo onyesha kama tukimtafuta Mungu kwa kweli tutampata sababu wote wanao mtafuta wanampata. Unaweza pia tumia kwao Luka 15 : 1-10 ; 19 : 10 ina onyesha kwamba Yesu anatafuta walio potea.
- Mda wa mimi kuokoka umekwisha pita, sasa haiwezekane tena. Kwa watu kama na hawa 2 Corinto 6 : 2 na umuonyeshe kwamba sasa ndio mda unaofaa kwa wokovu wako. Pia unaweza tumia Luka 23 : 39- 43 itakayo muonyesha kwamba mara nyingi ni wakati wa mwisho ndio Mungu ujibu kilio cha mwenye zambi. 2 Petro 3 : 9 inatuambia kwamba Mungu hapendi hata mumoja apotee ndio sababu anakuvumilia ili wote wafikie wokovu. Unaweza pia tumia Kumbukumbu la torati 4 : 30 – 31 ; Isaya 1 : 18 ; Ufunuo 22 : 17.

## 4. WANAO JIZANIA KUWA WATAKATIFU, WASIO NA DHAMBI

Kati ya watu wanao jizania kuwa hawana dhambi kunawale wanao tumainia matendo yao mazuri na hali yao ya maisha. Mara kwa mara utawajuwa kwa usemi ufuatao: Nimejitahidi kufanya mema, siye mwenye dhambi kuliko wenye kwenda kanisani, sijawai kuuwa, kuiba, kuzini na ninatendea watu wengi mema. Kwa watu kama na hawa, uwape wasome Wagalatia 3: 10 kwa kuwaonyesha kwamba wote wanao tumainia haki yao wenyewe, wako katika laana ya sheria, na kila asiye timiza mambo yote ya sheria hakuna tumaini kwake ya kuokolewa. Utatumia pia Yakobo 2: 10; Wagalatia 2: 16 na Warumi 3: 19- 20 ina onyesha wazi kwamba kwa matendo yake, hakuna mwanadamu anayeweza kuhesabiwa haki mbele za Mungu. Nilazima asome pia Yohana 16: 9 itakayo muonyesha kwamba kukataa kumpokea Yesu ndio dhambi kubwa na uzima wamilele unapatikana kwa njia ya Yesu peke yake kama inavyo andikwa katika Yohana 3 : 36.

Wengine kati ya watu wenye kujizania watakatifu husema Mungu ni mwema sana hata hawezi kuachilia mtu yeyeto katika moto. Mtu kama na huyu inabidi asome Waroma 2: 2, 4-5 na kumuonyesha kwamba kusudi la Mungu ni kwamba kupitia wema wake, yeye aokolewe ila si kwa kumuachilia aendelee kufanya dhambi. Na tukizarau wema wake katika kufanya dhambi, tutahukumiwa siku ya mwisho sababu tulipewa mda kuamini ila tulikataa. Hata kama yeye ni mwema Mungu atatupilia mbali wote walio mkataa mwana wake Yohana 8: 21 na 24; Matendo

3: 23. Pia 2 Petro 2: 4, 6, 9 na Luka 13: 3 inaonyesha namna gani Mungu aliye mwema anawatendea wanao endelea kufanya dhambi.

Wengine hujibia, ninajitahidi kuwa mkristo. Yohana 1: 12 inaonyesha kwamba si jambo la kujitahidi ao kufanya jambo la kumupendeza Mungu, ila ni kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha. Umupe pia asome Matendo 16: 31 ili aelewe kwamba Mungu hatuombe tujitahidi kuwa wakristo ila tumuamini Yesu. Unaweza pia kutumia Waroma 3: 23; Yohana 3: 36.

## 5. WAKRISTO WA JINA, WALIO ANGUKA

Kati ya wakristo wa jina kuna wale ambao hawana uakika ya wokovu wao, ambao wangali na shaka ya kuokolewa. Mbele ya watu wa aina hii, unaweza kuwapa wasome 1 Yohana 5: 13 itakayo muonyesha kama tunauhakika wa maisha ya milele. Unapowauliza ikiwa wameokoka ao ikiwa dhambi zao zimesamehewa, mara nyingi wanajibu: Ni Mungu peke yake ndie anajua. Nilazima wasome pia Yohana 1: 12 ina onyesha kwamba Yesu amewapa wote wanao muamini uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu. Unaweza pia tumia Yohana 3: 36 na umuulize: nani ndie, kufuatana na shairi hili, ana uzima wa milele? atajibu: yule anayemuamini mwana. Baadaye umuulize Je, unamuamini mwana? Akijibu Ndio, basi umuonyeshe kama hapashwe kuwa na shaka na wokovu wake. Shairi zingine za kutumia mbele za watu kama hawa ni hizi : Yohana 5 : 24 ; 1 Yohana 5 : 12 ; Matendo 13 : 39 na ataona lile Neno la Mungu limesema kuhusu wenye walimuamini Yesu.

Kwa wakristo ambao wamekwisha kuanguka utatumia Yeremia 2: 5 na kiisha uwaulize ubaya gani waliona kwa Yesu ili wamuache na kurudi nyuma katika maisha ya dhambi. Unaweza pia kumupa asome Yeremia 2: 13 na uwaulize ikiwa katika kumuacha Kristo hawatambue kama waliacha chemchem ya maji ya uzima? Unaweza pia tumia Yeremia 2: 19.

Kwa wakristo walioacha Kristo na ambao, baada ya kushiba dhambi, wanataka kumurudi, unaweza tumia Yeremia 3: 12 – 13 na 22 wataelewa kwamba Kristo yuko tayari kuwapokea waki mrudi. Hosea 14:1-4 imejaa maneno yanayo wa alika watu walio potea na inawaonyesha njia inayo warudisha kwa Mungu. Nilazima pia kuwaonyesha upendo mukubwa wa Mungu kwa walio rudi nyuma kupitia Isaya 43 : 22, 24, 25; 44 : 20-22 ; Yeremia 29 : 11 – 13; Kumbukumbu 4: 28- 31; 2 Mambo ya nyakati 15 : 4; 33: 1-9, 12 – 13 Itamuonyesha habari za mioyo iliyo rudi nyuma, lakini Bwana alizipokea zilipo mrudi. 1 Yohana 1: 9; Yeremia 3: 12-13; 2 Mambo ya nyakati itamsaidia nini anaweza kufanya kwa kumurudilia Kristo.

## 6. WAPAGANI WANAO MKANA MUNGU

Watu wa aina hii wanajulikana kwa namna mbalimbali. Unapowazungumzia utatambua kati yao kuna wale:

- Wanao mkana Mungu, kudharau wakristo na kuwachekelea. Kwa watu wa aina hii tumia 1 Wakorinto 1: 18 na akikujibu kwamba kwake yeye Biblia ni upuuzi, umujibu ndivyo Biblia yenyewe inasema kwamba ni ujinga kwa wale wanao potea. Unaweza pia tumia 1 Wakorinto 2 : 14; 2 Wakorinto 4: 3-4; 2 Watesalonika 2 : 10 – 12 ; Yohana 8: 21, 24.
- Wanao kana Mungu ila hawachekelee wakristo. Unaweza mupa asome Yohana 7: 17 inayo onyesha njia ipelekayo katika nuru.
- Wanao kana kuwepo kwa Mungu, unaweza wasomea Zaburi 14: 1 inayo onyesha nini Mungu anasema kuhusu wale wanao kataa kuwepo kwake na atatambua kama yeye ni mmoja wa wenye hawana akili. Unaweza pia tumia Zaburi 19: 2 na Waroma 1: 19 – 22.
- Wanao kataa kwamba Biblia si neno la Mungu, unaweza tumia Waroma 3: 23 itakayo muonyesha kwamba mashaka yake ao kukataa kwake hakuta punguza kitu. Matayo 24: 35 itamuonyesha pia kwamba neno la Mungu litadumu milele.
- Wanaoshakia maisha ya milele, utumie Ufunuo 21: 8; 19: 20; Matayo 10: 28; Luka 12: 5; Marko 3: 28- 29; 14: 21.
- Wanao shakia uMungu wa Kristo, utumie Matendo 10 : 36 ; 1 Wakorinto 2 : 8; Zaburi 24 : 8-10; Waebrania 1 : 8; Yohana 20: 28; Waroma 9: 5; Ufunuo 1 : 18; Isaya 44 : 6

## 7. WATU WANAO PENDA UBISHI

Unapo kutana na watu wenye kupenda ubishi katika huduma ya kuleta watu kwa Yesu, ni lazima kwanza kujua ni wa aina gani; sababu kati ya wenye kubishana, kuna wenye:

- Wanao nungunikia Mungu. Wengi kati yao watakuambia kwamba Mungu ni muuwaji na mwenye upendeleo. Mbele ya watu kama na hawa tumia Ayubu 41: 1-2 na Waroma 9 : 20. Mbele ya kumpa asome maandiko haya umuulize kwanza: Unaelewa dhambi kubwa unayotenda katika masemi yako? Baadaye umpe asome maandiko yale. Waebrania 12: 5, 7, 10, 11 inajibu wale wanao nungunika kwa ajili ya shida na majaribu yao wenyewe. Unaweza pia tumia Isaya 55 : 8-9. Ezekieli 33 : 11 itamuonyesha kwamba hata Mungu hafuraie kifo cha mwenye dhambi. 1 Timoteo 2 : 3-4; 2 Petro 3: 9 na Matayo 23: 37; Yohana 5: 40 itamsaidia kutambua kwamba Mungu hakuumba mwanadamu juu ya kumulaani.
- Wanao laumu mabishano kati ya shairi ya Biblia (Contradiction). Kwa watu kama hawa utatumia 1 Wakorinto 1: 18; 2: 14; 2 Wakorinto 4: 3-4; Danieli 12: 10; Waroma 11: 33-34; Yohana 7: 17; Zaburi 25: 14; Matayo 11: 25 na 2 Watasalonika 2: 10: 12.

- Wanao mchukia Mungu kwa kutoa mwana wake wapekee. Isaya 55: 8-9 na Waroma 11: 33 itakusaidia kuwajibu. Unaweza pia tumia Waroma 9 : 20.
- Wanao vunjika moyo kwa sababu ya mwenendo wa wakristo wakisema kwamba katika Kanisa kuna wanafiki wengi. Mbele ya watu wanao kujibu hivi, uwape wasome Waroma 14 : 4 na 12;  2: 1; Matayo 7: 1-5; Yohana 21 : 21 -22 na wata tambua kwamba wanapashwa kujihusisha na hali yao ya kiroho sio hali ya wengine. Utakuta wengine wenye kukataa kuamini sababu ya mabaya waliyotendewa na wakristo. Nilazima uwazungumzie ile Mungu anayo watendea na kuwaomba wasiangalie ile waliyotendewa na wanadamu. Kwa hivi uwape wasome Yeremia 2 : 5; Isaya 53 : 5; Waroma 5 : 6-8. Umuulize ikiwa sababu ametendewa mabaya na wakristo ndio inamruhusu kukataa baba yake anaye mutendea mema kila siku. Unaweza pia kumuonyesha umuhimu wa kusamehe watesi wetu ukitumia Matayo 18: 23 -35; Waefeso 4 : 31 – 32 ; Matayo 6: 14-15.

## 8. WATU WANAO PIGA HESABU

Watu wengi kati ya wale utakao pelekea habari njema wanapenda kurudisha wokovu wao kwa siku ingine wakisema nitaamini siku, juma, myezi ao miaka ijayo. Watu kama hawa ujibu: Namukubali Yesu ila hapana kwa sasa; nitakuja kesho, nitafikiri kwanza mbele ya kuamua.

Unapokutana na watu kama hawa, uwape wasome Isaya 55: 6; baadaye umuulize wakati gani ndio unafaa kwa kumtafuta Bwana? Umsaidie ajibu Ni sasa. Unaweza pia kutumia Mezali 29: 1; Matayo 25: 10-12; Mezali 27: 1; Yakobo 4: 13 – 14; Ayubu 36: 12; Luka 13 : 24, 28.

Wengine watakujibu wanachunga siku yao ya wokovu. Kwa watu kama hawa uwape 2 Wakorinto 6: 2; Waebrania 3: 15.

Kwa wale wanaojibu kwamba wao wangali vijana wataokoka saa watakuwa wazee, uwape Muhubiri 12 : 1, 3; Matayo 19: 14 na 18: 3 inayo onyesha kwamba ujana ndio muda unao faa kwa kumtafuta Mungu. Tumia pia Mezali 29: 1. Kwa wale wanao sema kwamba wanapenda dunia sana, uwape wasome Luka 14: 33; 12: 16- 21 na 1 Yohana 2 : 15 - 17

**KWA MWISHO**

Huduma ya kuleta watu kwa Yesu ni ya muhimu sana. Biblia inaonyesha namna gani mbinguni kuna karamu mwenye zambi mmoja anapo okoka.

Ni lazima kufahamu ya kwamba huduma ya mwinjisti inahusika na kupasha habari njema na kugeuza moyo wa Mtu ni kazi ya Roho mtakatifu. Kwa hivi, ni lazima mwinjilisti afuate shauri zifuatazo kwa kufaulu katika huduma yake:

1. Ikiwezekana, ni vizuri kuzungumza na mtu kuhusu wokovu mukiwa ninyi wawili tu. Mara nyingi watu hupendelea kuwa mbali na watu wengine ili wawe huru kujieleza;
2. Nilazima kutumikisha uwezo wa Roho Mtakatifu kwa kuleta watu kwa Mungu. Elimu, masomo na hali ya mwinjilisti haviweze peke yao kuleta watu kwa Yesu;
3. Si vizuri kwa mwinjilisti kutaja ao kusoma mwenyewe maandiko matakatifu. Ni vizuri mtu tunayehubiri asome mwenyewe Biblia na mwinjilisti akazie maneno anayo ya soma;
4. Mara nyingi ni vizuri kutumia andiko moja tu pahali pa maandiko mingi;
5. Haifae kusahau kusudi la mazungumzo: Wokovu wa mtu unaye zungumza naye. Kwa hivi mwinjilisti ataepuka mabishano mingi ao kuzungumzia mada ingine;
6. Ni ya lazima sana kuepuka mizaa na michezo wakati tunapenda kuleta watu kwa Kristo. Mavalio yetu, mwendo wetu na hali yetu inapashwa iwe yenye kushuhudia wokovu wetu;
7. Inabidi kuwa mvumilivu. Kuleta mtu kwa Yesu inaomba mda na haifae kuwa na hasira;
8. Mwinjilisti anapashwa kuepukana na mabishano ao magonvi ni mtu anayependa kuleta watu kwa Yesu;
9. Inafaa kuepuka kufanya kazi hii kwa haraka. Ni lazima mtu aelewe kwamba unajiusisha na hali yake na uko tayari kutoa mda wako kwa ajili yake;
10. Ikiwezekana umuombe mtu anayekubali Kristo kukunja magoti yake kwa ajili ya maombi. Hata kama anakataa, ni lazima, ikiwezekana, uombe naye hata juu ya maitaji yake;
11. Wakati unapofikiri kwamba unashindwa kuleta mtu kwa Yesu, ni lazima uonyeshe mtu yule kwa Mungu katika maombi ili aendelee kugusa roho yake baada ya kumu hubiri;
12. Mbele ya kuachana na mtu anaye mkubali Kristo, ni lazima umuongoze namna ya kuishi maisha mapya:

- Ku mkiri Yesu kila mara Waroma 10 : 10-11; Matayo 10 : 32-33;
- Kujifunza kila siku neno la Mungu 1 Petro 2 : 2; Matendo 20 : 32; 2 Timoteo 3 : 14 -17; Matendo 17 : 11;

- Kuomba kila siku, kila wakati wa shida Luka 11 : 9 – 13; 22 : 40; 1 Watesalonika 5 : 17;
- Kuepuka dhambi zote, kuishi maisha ya utakaso 1 Yohana 1 : 6-7; Waroma 14 : 23; Yohana 14 : 21;
- Kujiunga na kikundi cha wakristo wengine, kujiunga na Kanisa la mahali Waefeso 4: 12 – 16; Matendo 2 : 42 – 27; Waebrania 10 : 24 – 25;
- Afanye huduma moja katika Kanisa Matayo 25 : 14 -30;
- Akidanganyika na kuanguka katika dhambi, asivunjike moyo; atubu (aombe msamaa kwa Mungu) na aendelele mbele 1 Yohana 1: 9 ; Wafilipi 3: 13 – 14.

13. Baada ya kuleta mtu kwa Yesu ni lazima ufatilie maisha yake ya kiroho, usimuache kabla haja komaa kiroho.

*Basi, kwa yeye anaye tuita kumutumikiya na anaye tupatiya uwezo wa kumtumikiya ziwe sifa utukufu milee na milele, Amina.*